

**HOTUBA YA MHE. CHARLES MAKONGORO NYERERE,  
MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA KUMKABIDHI  
MWENGE WA UHURU 2023 MHE. DKT. FRANCIS  
KASABUBU MICHAEL MKUU WA MKOA WA SONGWE  
KATIKA KIJIKI CHA KAMSAMBA WILAYA YA MBOZI MKOA  
WA SONGWE TAREHE 02 SEPTEMBER, 2023**

- *Mhe. Dkt. Francis Kasabubu Michael, Mkuu wa Mkoa wa Songwe,*
- *Ndugu Abdalla Shaib Kaim, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, 2023.*
- *Ndugu Wakimbiza Mwenge Kitaifa,*
- *Makatibu Tawala wa Mikoa ya Rukwa na Songwe,*
- *Ndugu Viongozi wa CCM wa Mikoa ya Rukwa na Songwe,*
- *Waheshimiwa Wabunge*
- *Wahe. Wakuu wa Wilaya Kutoka Mikoa ya Rukwa na Songwe,*
- *Wajumbe wa Kamati za Usalama za Mkoa wa Rukwa na Songwe,*
- *Maafisa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais,*
- *Makatibu Tawala wa Wilaya za Rukwa na Songwe,*
- *Waheshimiwa Madiwani*
- *Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,*
- *Kamati za Amani Rukwa na Songwe*

- ***Ndugu Wanahabari,***
- ***Ndugu Wananchi,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ...**

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe,*** Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetulinda na kutukutanisha sote tukiwa na Afya njema pamoja na wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa wakiongozwa na ***Abdalla Shaib Kaim.***

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,*** Tuliupokea Mwenge wa Uhuru 2023, Kiongozi wa Mbio za Mwenge na Wakimbiza Mwenge Kitaifa jumla yao wakiwa sita (06) tarehe **29 Agosti, 2023** toka Mkoa wa Katavi ukiwa salama, unawaka, unang'aa, unameremeta. Mwenge wa Uhuru katika Mkoa wetu umetembea umbali wa Kilomita **778.8** ambapo umepata taarifa za uhifadhi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji, umetoa elimu kwenye masuala ya VVU/UKIMWI, Lishe bora, Malaria, Mapambano dhidi ya Rushwa na Mapambano dhidi ya Dawa za kulevya,

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,*** umetembelea **miradi 26;** ambapo **miradi 09 imewekwa mawe ya msingi, miradi 07 imezinduliwa na Mradi 10 imekaguliwa.**

Kati ya Miradi yote 26 iliyotembelewa hakuna mradi uliokataliwa. Nitumie fursa hii kukuhakikishia kuwa tumeyapokea maelekezo yote yaliyotolewa na Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa Mwaka 2023 kwenye miradi yote na tunaahidi kuyafanyia kazi haraka iwezekanavyo.

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,*** Katika maeneo yote ya mkesha wa Mwenge wa Uhuru, 2023 tumefanikiwa kufanya Upimaji wa VVU/UKIMWI na Malaria kama ifuatavyo:-

Waliopima VVU/UKIMWI		Walio kutwa na maambukizi	Hali ya lishe Waliopimwa		Walio kutwa na lishe duni	Waliopima Malaria		Walio kutwa na Malaria	Uchangiaji wa Damu Salama
Me			Me			Me			Zilipatika na Unit ..... za Damu
Ke			Ke			Ke			
Jml									

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe,*** Wakati nahitimisha hotuba yangu, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa, 2023 chini ya Kiongozi wao mahiri, shupavu na mwenye ushauri Ndugu **Abdalla Shaib Kaim** pamoja na timu yake ya vijana sita (6) mahiri, wakakamavu na wanaojituma, ambao waliambatana **na Maafisa wanne (4) kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais** kwa ushirikiano waliotupatia katika kipindi chote ambacho Mwenge wa Uhuru ulikuwa

Mkoani kwetu. Kwa namna ya pekee niwashukuru sana Wananchi wa Mkoa wa Rukwa pamoja na viongozi mbalimbali kwa ushirikiano wao walionipatia hadi tulipofanikiwa kumaliza salama kukimbiza Mwenge wa Uhuru kwenye Mkoa wetu. **Asanteni sana.**

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe,** Naomba sasa nikukabidhi Maafisa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais ambao ni;

1. ....
2. ....
3. ....
4. ....

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe,** Baada ya kukukabidhi Waratibu wa Wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa sasa nikukabidhi wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa sita (06) Wakiwa na Afya njema, Wanang'aa na kumeremeta kama ifuatavyo:-

1. Ndugu Juma Silima Sheha - Kaskazini Unguja
2. Ndugu Martin Michael Mkanga- Mtwara
3. Ndugu Atupokile Elia Mhalila – Dodoma
4. Ndugu Zainabu Hemedi Mbetu - Kusini Unguja
5. Ndugu Emmanuel Jackson Hondi– Manyara

6. Ndugu **Abdalla Shaib Kaim** – Kiongozi wa Mbio za  
Mwenge wa Uhuru Kitaifa - Kaskazini Pemba

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa***, Sasa nitumie fursa hii  
kukukabidhi rasmi Mwenge wa Uhuru ukiwa unang'aa,  
unameremeta na ukiwa salama salimini.

**Mwenge wa Uhuru Hoyeeeeeee!!!!**

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**